

Upatikanaji wa Programu za Wavu Salama (NSP) kwa Familia za Wahamiaji wa Kikongo wa North Carolina

Mitazamo kutoka kwa Washiriki wa Kikundi Lengwa

Diana Guelespe, Hamutal Bernstein, Jennifer M. Haley, Sofia Hinojosa, Luis Gallardo, Hannah Gill, na Krista Perreira

Timu ya Urban Institute na UNC-Chapel Hill ilifanya utafiti mwaka 2022 na 2023 ili kuchunguza vizuizi vya upatikanaji wa programu za wavu salama (safety net programs) za serikali kuu za afya na lishe kama [Medicaid na SNAP](#) kwa wahamiaji wenye ustahiki na wanafamilia wenye hali mchanganyiko katika North Carolina na kubaini sera na taratibu ambazo zitapunguza hali ya kukosekana kwa usawa.

Tulifanya mahojiano 42 na wadau kutoka [mashirika ya HHS, CBO, mashirika yanayoshughulikia makazi ya wakimbizi, vituo vya afya vinavyotambuliwa na serikali kuu, na mashirika mengine yanayohudumia wakimbizi](#) yanayofanya kazi sehemu mbalimbali za jimbo au wilaya za Catawba, Forsyth, Pitt, au Wake.

Kikao cha mtandaoni cha makundi manne lengwa kilifanyika kwa lugha za [Kihmong, Kispaniola, na Kiswahili](#), na vikao viwili vya mtandaoni vya kusikiliza jumuiya vilisaidia kukusanya mawazo kutoka kwa wadau wa jumuiya kuhusu matokeo ya utafiti husika.

Uundaji wa [zana ya data ya jimbo zima](#) ulitoa data ya kidemografia kwa ngazi ya wilaya kuhusu familia za wahamiaji.

Katika miongo ya hivi karibuni, idadi ya wahamiaji mbalimbali wa North Carolina imekua, huku familia za wahamiaji zikiishi katika jumuiya za vijijini na mijini kote jimboni.¹ Hii inajumuisha familia za wahamiaji na wakimbizi kutoka nchi mbalimbali zinazozunguma lugha nyingi tofauti tofauti. Wahamiaji wanakabiliwa na vizuizi vya ustahiki wa mafao ya umma kulingana na hali yao ya uhamiaji. Aidha, baadhi ya wahamiaji waliacha kujiandikisha wao wenyewe au watoto wao katika programu za wavu salama, kama vile Medicaid na mafao ya lishe, ambazo zinatolewa na mashirika ya Afya na Huduma za Binadamu (HHS) katika ngazi ya wilaya. Matokeo yake, wao na familia zao wapo katika hatari kubwa ya chakula na ukosefu wa usalama katika huduma za afya.

Kikundi lengwa cha Juni 2023 kilichokuwa na washiriki 12 wa jumuiya ya Wakongo wanaozunguma Kiswahili wa North Carolina kilijumuisha watu walioishi Marekani kati ya miezi minne na miaka minne. Wote waliwasili kama wakimbizi. Tofauti na wahamiaji wengine, wakimbizi wote wana ustahiki wa programu za serikali kuu za wavu salama wanapowasili Marekani na wanapata usaidizi wa kujiandikisha nazo kutoka kwa watoa huduma ya makazi ya wakimbizi. Hata hivyo, usaidizi huenda usipatikane kwa wingi kadri muda unavyopita wakati wakimbizi wanapofanya michakato ya kudumisha au kurejesha mafao. Katika kundi lengwa, tulisikia kwamba lugha ilikuwa kizuizi chao kikubwa cha ufikio wa programu za wavu salama. Pia waliangazia changamoto za kutoa nyaraka za kuthibitisha kipato, makazi, na matakwa ya mchakato wa maombi. Mapendekezo yao kwa HHS kuhusu kupunguza vizuizi hivi yalijumuisha kutoa taarifa zote kuhusu programu kwa Kiingereza na Kiswahili, kuajiri wakalimani wa Kiswahili, na kuruhusu wafanyakazi wa mashirika ya jumuiya (CBO) kutenda kwa niaba ya waombaji.

VIKWAZO VYA LUGHA KUWASILIANA NA WAFANYAKAZI WA MASHIRIKA

Washiriki waliripoti kwa wingi ukosefu wa tafsiri na ukalimani kwa Kiswahili wakati wa kuwasiliana na wafanyakazi wa HHS wa wilaya. Wengi walipendelea kuwasiliana na mashirika mahalia ya HHS ana kwa ana, badala ya simu au mtandaoni, na mara nyingi baadhi ya wanajumuia hawakujua kusoma na kuandika kwa lugha yao wenyewe. Hakuna aliyewahi kuona nyenzo zozote zilizoandikwa kwa Kiswahili katika shirika la HHS katika wilaya yao. Waliripoti kupokea mawasiliano yote kutoka kwa HHS kwa Kiingereza na Kihispania tu, hata pale ambapo wafanyakazi wa HHS wakijua hawazungumzi lugha hizi. Pia waliripoti ukosefu wa matumizi ya huduma za kitaalamu za ukalimani wakati wa kupiga simu ofisi ya HHS na kupata shida katika kutafuta na kuzuru majengo ya serikali kutokana na kizuizi cha lugha. Ili kuondokana na kizuizi hiki, washiriki waliripoti kuja na meneja wao wa shirika la makazi mapya na kutumia watoto wao kama wakalimani walipotembelea ofisi za HHS. Mkalimani wa lugha ya Kiswahili ambaye aliongoza kundi lengwa alielezea mitazamo ya baadhi ya washiriki kama ifuatavyo:

Kizuizi cha lugha ni jambo kubwa. Wakati mwingine wanatumia watoto wao lakini huenda watoto wao wana shughuli nyingi au wapo shuleni.... Wanataka kutuma maombi lakini inabidi wasubiri mtu wa kuwasaidia, labda hadi watoto wao watakapopatikana.

KUTIMILIZA MATAKWA YA UANDIKISHAJI KUPITIA USAIDIZI USIOTOSHA

Ingawa washiriki wa kikundi lengwa walibaini kuwa walipata usaidizi kutoka kwa mashirika ya makazi mapya wakati wa kutuma maombi ya kwanza, walikosa usaidizi huo walipohitaji kurejesha mafao au hati za ziada ziliombwa ili kusalia kuandikishwa. Waliripoti kwamba kutimiliza michakato ya uandikishaji, hasa kuwasilisha nyaraka zinazohitajika, ilikuwa changamoto kubwa ya kupata programu husika. Washiriki kadhaa walionesha kuchanganyikiwa na idadi ya mara ambazo walitakiwa kurudi katika ofisi za shirika kuwasilisha makaratasi, muda uliochukua kupata majibu kutoka kwa mashirika, na ugumu wa kutambaza nyaraka kielektroniki. Kati ya aina za nyaraka ambazo zilikuwa zenye changamoto zaidi ni risiti za malipo, ambazo zilikuwa ngumu kufikiwa kutoka kwa mifumo ya mtandaoni, na mikataba ya upangishaji. Ikijumuishwa na uwezo mdogo wa kusoma na kuandika Kiingereza, waliona mchakato wa kuwasilisha nyaraka kuwa mzigo mzito, ambao unafadhaisha, na kukatisha tamaa.

Changamoto nyingine ni ukosefu wa usafiri wa kuhudhuria miadi ya HHS, hasa katika hatua za awali za kuwasili Marekani wakati bado hawana gari au hawajui jinsi ya kutumia mifumo ya mabasi mahalia. Changamoto za kupata watoa huduma na maduka ya dawa ambayo yanakubali Medicaid pia ziliibuliwa, huku mshiriki mmoja akionesha shaka kuhusu ufanisi wa Medicaid na kurejelea bili ya \$800 waliyopokea wakati daktari wao alipokataa kupokea bima ya Medicaid. Washiriki pia waliuliza maswali kuhusu kutojua jinsi ya kutuma maombi na wasiwasi kwamba hawatapata mafao kwa vile walisikia kuhusu wanajumuiya wengine waliojandikisha bila mafanikio. Tofauti na washiriki wa kikundi lengwa cha wanaozungumza Kihispania walioibua wasiwasi kama vile "tozo ya umma" kama chanzo cha hofu na kizuizi kwa uandikishaji wa programu za wavu salama, washiriki wa vikundi vya Wakongo² na Wahmong hawakutoa wasiwasi wa uhamiaji.

FUMBUZI ZILIZOTOLEWA

Wanapotuma nyaraka, ningependekeza—kama vile wanavyotuma [nyaraka] kwa Kiingereza na Kihispania—wafanye hivyo pia kwa Kiingereza na Kiswahili. Kwa njia hiyo, tunapokea [barua], tunajua wanachosema Inapaswa kupatikana kwetu kwa lugha tunayoielewa.

Washiriki walipendekeza ofisi za HHS zitekeleze yafuatayo wakati zinapohudumia jumuiya inayozungumza Kiswahili:

- Mawasiliano yote yatumwe kwa Kiingereza na kwa lugha ambazo wateja wanapendelea, yaani Kiswahili, kama inavyofanywa kwa jumuiya inayozungumza Kihispania, ili kuhakikisha kwamba wanaweza kusoma na kutenda inapohitajika.
- HHS inapaswa kuajiri wafanyakazi wanaozungumza lugha zile zile kama wateja wao, ikiwemo Kiswahili, na kuoanisha wateja na wafanyakazi wenye uwezo sawa wa lugha. Wakalimani wa ana kwa ana wanapaswa pia kuajiriwa ili kusaidia wateja ambao hawawezi kusoma au kuandika kwa lugha yao ya asili.
- Ofisi za HHS ziruhusu CBO kuwasiliana na kutenda kwa niaba ya wateja wao, hasa wale wenye vizuizi vya lugha. Mashirika ya makazi ya wakimbizi yanayohudumia jumuiya inayozungumza Kiswahili yanaweza kuelezea kwa ufasaha zaidi mchakato na kipi kinahitajika kwa wateja wao.

CHAPISHO LA ZIADA

Kuunga Mkono Familia za Wahamiaji za North Carolina: Kushughulikia Vizuizi na Kuendeleza Fumbuzi kwa Programu za Wavu Salama zilizo Jumuishi Zaidi

Hamutal Bernstein, Jennifer M. Haley, Diana Guelespe, Sofia Hinojosa, Luis Gallardo, Hannah Gill, and Krista Perreira urban.institute.org/3tBksPb

¹ Krista M. Perreira and Lisa Carlson. 2023. *The Immigrant Community in North Carolina*. Chapel Hill, NC: Carolina Population Center.

² Diana Guelespe, Hamutal Bernstein, Jennifer M. Haley, Sofia Hinojosa, Luis Gallardo, Hannah Gill, and Krista Perreira. 2023. "Access to Safety Net Programs for North Carolina's Spanish-Speaking Immigrant Families: Perspectives from Focus Group Participants." Washington, DC: Urban Institute. Diana Guelespe, Hamutal Bernstein, Jennifer M. Haley, Sofia Hinojosa, Luis Gallardo, Hannah Gill, and Krista Perreira. 2023. "Access to Safety Net Programs for North Carolina's Hmong Immigrant Families: Perspectives from Focus Group Participants." Washington, DC: Urban Institute.